# KWA NINI MUNGU ANARUHUSU MATESO?

Bill Pinto



***Ni kwa nini Mungu mwenye upendo anaruhusu dhambi iwepo?***
***Ni kwa nini kuna maumivu na mateso?***
***Ni kwa nini Mungu haingilii kati?***

Maswali kama haya hujitokeza zaidi nyakati za huzuni, msukosuko wa kihisia, na majaribu yanapotokea. Kwa kweli, swali la ni kwa nini Mungu mwenye upendo anaruhusu maumivu na kuteseka ni mojawapo ya mambo makuu yanayopinga Ukristo. Kwa mfano, swali hilo ndilo lililomsumbua sana mama yangu, ambaye alikuwa amehuzunishwa sana na hali ya watoto wanaoteseka. Kwa hakika, swali hili limewafanya watu wengi watilie mashaka Neno la Mungu na kuiacha imani yao ya kuwa Wakristo na kuwa watu wenye mashaka na wasioamini.

Kabla ya kuanza kujifunza somo kama hili, kuna kanuni chache muhimu za kuzingatiwa. Kwa kuanza, mtu anahitaji kulitathmini suala hilo kwa uaminifu, bila upendeleo au mawazo yanayokinzana. Kwa mfano, hebu tuchukulie kwamba unamtuhumu mtu vibaya kulingana na mambo ambayo si sahihi na yanayopotosha. Ni wazi hukumu yako itakuwa na kasoro kwa kuwa inategemea misingi ya uongo. Ni jukumu lako kuujua ukweli ili uweze kufanya uamuzi wenye uaminifu. Vivyo hivyo, ni muhimu kuushughulikia utafiti huu kwa uwazi na bila mawazo yanayokinzana. Zaidi ya hayo, kwa kuwa ni tabia ya Mungu inayozungumziwa, mhusika anapaswa kulisoma Neno la Mungu ili kupata majibu.

Unaweza kulikumbuka jina la Charles Templeton. Templeton alikuwa ni muinjilisti maarufu wakati wa Billy Graham. Kama ilivyokuwa kwa Graham, Templeton alikuwa maarufu sana na aliuvutia umati mkubwa akiwa kama mhubiri ambaye ni kijana. Hata hivyo, Templeton aliiacha imani ya Kikristo na hata kuandika kitabu kilichoikosoa Biblia. Sababu kuu ya ukengeukaji wake ilikuwa ni swali tunalolizungumzia leo hii. Zaidi ya hayo, Templeton aliamini kwamba Mungu angewaweka jehanamu iwakayo milele zaidi ya nusu ya watu ambao wamewahi kuishi. Kwa kawaida, imani hiyo ilimfanya amchukie sana Mungu na Ukristo. Bado imani hii ni upotoshaji wa ukweli. Jehanamu iwakayo milele haifundishwi kwenye Biblia. Badala yake, ni fundisho la uongo lililobuniwa na Shetani ili kuidharau tabia halisi ya Mungu. Mafundisho haya

yamewafanya watu wengi kuwa waliokengeuka kuliko mafundisho mengine yoyote ya uongo. Licha ya jambo hili, si vigumu kuufichua ukweli kuhusu kuzimu pale unapoisoma Biblia kwa umakini. Lakini, licha ya kuwa ni Mkristo muinjilisti aliyefundisha Biblia, Templeton alishindwa kuutafuta ukweli. Kwa sababu hiyo, alijikuta akivunjwa moyo na swali la ni kwa nini Mungu mwenye upendo anaruhusu maumivu na kuteseka.

Bila shaka, hakuna ubaya wa kuuliza swali hili. Mungu anataka tuipate dhana iliyo wazi zaidi ya tabia Yake halisi. Hata hivyo, wengi huuliza swali hili wakiwa bila ya hamu ya kulijua jibu. Badala yake, kuhoji kwao kunatokana na kutafuta mahali pa kukaidi na kuipinga Biblia na Ukristo. Kwa hakika, pingamizi hili mara nyingi huibuliwa na watu wale wale wanaomkataa Mungu kwa sababu ya unafiki, ufisadi, na uovu unaofanyika kwenye kanisa. Lakini hata hivyo mambo haya ya wazi yasiyo ya haki si sababu ya kutoa hukumu juu ya Mungu na Neno Lake. Tunahitaji kuuliza maswali kwa uaminifu, na kutafuta majibu kwa nia njema ya kuujua ukweli. Hii inamaanisha kujenga hoja kutoka kwenye sababu hadi kwenye matokeo yake. Kwa kuzingatia kanuni hii, mhusika ataona kuwa si vigumu sana kupata majibu.

Fikiria kisa kifuatacho. Mwanaume mmoja anamaliza kazi zake na kuelekea nyumbani, anasimama kwenye baa njiani ili kunywa pombe. Anakunywa sana pombe lakini bado anachagua kuendesha gari lake kuelekea nyumbani. Katika safari yake, anapoteza umakini wa chombo chake na kuua familia isiyo na hatia. Ni nini kilichosababisha kifo cha familia hiyo? Na ni nini kilichosababisha kuteseka na huzuni kwa wapendwa wao? Misiba na huzuni iliyoambatana nayo ilisababishwa na chaguo la mtu mmoja kutenda mambo bila ya kuwajibika.

Huenda wengine wakateta kwamba kwa kuwa Mungu ni muweza wa yote, angeweza kuzuia ajali hiyo isitokee. Wanasema hivi kana kwamba Mungu huwa haingilii kati hata kidogo. Ukweli ni kuwa Mungu anafanya kazi kila wakati ili kutulinda, kutustawisha, na kuokoa maisha yetu. Halali wala kusinzia. Kwa kila hadithi ya huzuni unayoisikia kuhusu mtu ambaye amempoteza mpendwa wake, unaweza kusikia hadithi ya mtu ambaye—ikiwa sio Mungu na uwepo Wake—asingekuwa hai.

Biblia imejaa ahadi za ulinzi na utunzaji Wake, na ushiriki wa malaika Wake wanaotulinda na kutustawisha kila siku.

Walakini, tuseme kwamba kila wakati jambo la kutisha lilipokuwa karibu kutokea kutokana na kutowajibika kwa mtu, Mungu akaingilia kati. Matokeo yake yangekuwa ni nini? Ingehamasisha tabia mbaya kuendelea, kwa kuwa hakuna ambaye angejua matokeo ya mambo yake mabaya.

Katika ulimwengu huu, tunaoneshwa vielelezo vya wazi vya madhara ya kuvuta sigara na kuendesha gari huku ukiwa umelewa. Tunaoneshwa picha na namna watu wanavyoteseka hospitalini. Hii ina lengo la kutuonesha waziwazi matokeo ya kuendeleza mazoea mabaya na kufanya maamuzi mabaya.

Kama nilivyoelezea, mara nyingi Mungu huingilia kati. Hata hivyo inabidi pia aturuhusu kuvuna mavuno ya matendo yetu kwa matumaini kwamba tutajifunza kutoka kwenye makosa hayo. Hii ni kanuni muhimu kuielewa. Kwa mfano, usiku ule ule ambapo dereva mlevi katika mfano wetu aliua familia isiyo na hatia, maelfu ya watu wengine walimaliza kazi zao na kurudi nyumbani wakiwa salama. Katika hali nyingi, tuna chaguzi za kufanya katika hali hizo. Tunaweza kuchagua kuwajibika kwenye matendo na tabia zetu, au tunaweza kuchagua kutowajibika. Hilo la pili litaleta matokeo, na Mungu anataka tujifunze kutoka kwenye makosa. Kwa hiyo, kabla ya kuuliza ni kwa nini Mungu aliruhusu jambo fulani litokee, fikiria kwanza kilichosababisha kuteseka huko. Hii ndio maana ya kuhoji sababu kwa uwazi kutoka kwenye sababu ya jambo hadi kwenye matokeo yake.

Hatimaye, sababu ya kwa nini mambo haya yote yatokee ni kutokana na dhambi. Dhambi ndiyo chanzo cha mateso, ukosefu wa haki, ukatili na matatizo yote kwenye ulimwengu huu. Mungu alipoumba dunia na wanadamu, ilikuwa ni kamilifu. Binadamu na wanyama waliishi kwa mapatano kamili pamoja na Muumbaji wao. Na mwanadamu alikuwa ni taji la uumbaji wa Mungu, kwa maana tuliumbwa kwa sura na mfano wa utukufu wa Mungu. Hakukuwa na dhambi na hakukuwa na mateso. Kisha, mwanadamu akachagua kutomtii Mungu. Kwa hivyo,

dunia ililaaniwa. Asili ya mwanadamu ilipotoshwa, na mateso na kifo vikaingia katika sehemu ya maisha yote duniani. Mateso haya yameendelea kuongezeka tu. Ni udanganyifu kuamini kwamba ulimwengu unaboreshwa. Sio tu kwamba uchunguzi na sababu zinatuambia kuwa hayo si kweli, lakini Biblia pia inasema tofauti. Kabla ya kurudi kwa Kristo, Biblia inatuonya kwamba ulimwengu utazidi kuwa mbaya zaidi na zaidi (2 Timotheo 3). Na kadri dhambi inavyoongezeka, mateso na kifo pia vitaongezeka.

Tukirejea historia kwenye kitabu cha Mwanzo, tunaona kwamba tukio la kwanza la kifo cha mwanadamu ilitokea wakati Kaini (mwana wa kwanza wa Adamu), alipomuonea wivu Abeli, nduguye mdogo. Kaini alikuwa na nia mbaya kwa Abeli na akamuua. Tukio hili iliamsha hali ya mauaji ya kwanza kwa wanadamu. Kutokana na kifo hicho cha kwanza tumeshuhudia vita vya dunia, mauaji ya kimbari na vitendo vikubwa vya kigaidi ambavyo havijafika ukomo wa kuendelea kutokea. Kuna umuhimu mdogo kwenye maisha ya mwanadamu. Yote haya ni kwa sababu ya dhambi. Dhambi ni nini? Tafsiri pekee ya dhambi iliyotolewa kwenye Biblia nzima ni hii:

> 1 Yohana 3:4 Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa, dhambi ni uasi wa sheria.

Dhambi ni uvunjaji wa sheria. Sheria ni nini? Kwenye Yakobo 2:8-11 tunasoma:

> Yakobo 2:8 Lakini mkiitimiza ile sheria ya kifalme kama ilivyoandikwa, Mpende jirani yako kama nafsi yako, mwatenda vyema.
> 2:9 Bali mkiwapendelea watu, mwafanya dhambi na kuhukumiwa na sheria kuwa wakosaji.
> 2:10 Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote.
> 2:11 Kwa maana yeye aliyesema, Usizini, pia alisema, Usiue. Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa mvunja sheria.

Sheria ni amri kumi, kama inavyoonyeshwa na mifano ambayo Yakobo anaitoa katika mstari wa 11. Si sahihi kusema kwamba wewe si mwenye

dhambi kwa sababu tu hauui. Yakobo anafichua kwamba kwa kuvunja hata amri mojawapo, una hatia ya dhambi zote. Kwa hiyo, sheria inakuhukumu wewe kuwa ni mwenye dhambi. Na ni dhambi—uvunjaji wa amri kumi—ambayo huleta mateso.

Katika hatua hii, mtu anaweza kufikiria majanga ya asili, na kuuliza yanahusiana nini na matendo ya mwanadamu. Kama ilivyotajwa awali, hakukuwa na dhoruba, mafuriko, moto wa nyikani, au matetemeko ya ardhi wakati Mungu alipouumba ulimwengu. Kwa hivyo iwe ni moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, mateso yote yanarudi kwenye uasi wa mwanadamu dhidi ya Mungu; uasi wa mwanadamu kwenye sheria yake. Na kila mmoja wetu ana sehemu yake ya kuwajibika. Kwa maana Mungu alipouumba ulimwengu, ilikuwa kamilifu. Hata mvua haikunyesha juu ya nchi kabla ya dhambi kutokea. Ona katika kitabu cha Mwanzo jinsi dunia ilivyobuniwa kwa njia ya ajabu sana.

> Mwanzo 2:5 hapakuwa na mche wa kondeni bado, wala mboga ya kondeni haijachipuka bado, kwa maana BWANA Mungu hajainyeshea nchi mvua, wala hapana mtu wa kuilima ardhi;
> 2:6 ukungu ukapanda katika nchi, ukatia maji juu ya uso wote wa ardhi.

Kifungu hiki kinafichua uzuri wa bustani ya Edeni, na jinsi mazingira yalivyoshirikiana kikamilifu na mwanadamu. Wakati mwanadamu alipopaswa kuitunza bustani, hapakuwa na miiba au ardhi yenye miamba ili kulazimisha uwepo wa kazi ngumu. Kazi hiyo ilikuwa ya kufurahisha, na haikufanya 'kutokwa na jasho usoni'. Zaidi ya hayo, ukungu mzuri ulikuja kila asubuhi ili kumwagilia maji kwenye dunia. Adamu alipofanya dhambi, dunia ililaaniwa. Dhambi ya kudumu na isiyosamehewa ndipo ikasababisha mafuriko, ambayo yalibadilisha hali ya angahewa la dunia, na kusababisha maafa ya asili kutokea tangu wakati huo. Angalia kutoka kwenye kifungu hapa chini jinsi mafuriko yalivyokuwa makubwa na ya kutisha sana.

> Mwanzo 7:11 Katika mwaka wa mia sita wa maisha ya Nuhu, mwezi wa pili, siku ya kumi na saba ya mwezi, siku ile chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu, madirisha ya mbin-

guni yakafunguka.

Haikuwa tu mvua kutoka mbinguni ambayo ilileta gharika, bali bahari kubwa ya sehemu ndogo ya nchi kavu ambayo ilipasuka na kutoka chini ya ardhi. Hii ilibadilisha sehemu ya chini ya dunia na ni kwa sababu hii kuna mistari ya mpasuko kwenye ardhi, ambayo bila shaka ina jukumu kubwa kwenye matetemeko ya ardhi na tsunami tunazoziona leo hii. Fikiria vichwa vifuatavyo vya mada ambavyo wanasayansi wanatambua uhusiano uliopo kati ya mvua kubwa na matetemeko ya ardhini.

> "Mvua Kubwa Inaweza Kusababisha Matetemeko Makubwa ya Ardhi" — *National Geographic*

> "Ni kwa nini mvua kubwa inaweza kusababisha matetemeko ya ardhi" — *The Times UK*

> "Ni kwa nini tetemeko la ardhi la Haiti linaweza kuwa si janga la asili" — *Independent UK*

Zingatia pia dondoo zifuatazo kutoka kwenye makala iliyoandikwa na maprofesa watatu wa elimu ya jiofizikia yenye mada: 'Mvua ya California Inaweza Kuibua Maswali Mapya Kuhusu Nini Husababisha Matetemeko ya Ardhi'.

> "…kuyaelekeza maji kwenye visima—ama kwa ajili ya kutupa taka au kuondoa mabaki ya mafuta kutoka kwenye hifadhi zilizopungua—kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha matetemeko ya ardhi…

> ...Leo hii, matetemeko ya ardhi yanayosababishwa na wanadamu yanatokea kwa kiwango kikubwa zaidi. Matukio ya karne iliyopita yameonesha uchimbaji madini ni mojawapo ya shughuli nyingi za viwandani ambazo zinaweza kusababisha matetemeko ya ardhi makubwa kwa kiasi cha kutosha kusababisha uharibifu mkubwa na kifo. Kuzijaza hifadhi za maji ya mabwawa, uchimbaji wa mafuta na gesi, na uzalishaji wa nishati ya jotoardhi ni baadhi tu ya

shughuli za kisasa za viwandani zinazoonesha kusababisha matetemeko ya ardhi."

"…Siku hizi, matetemeko ya ardhi yanayotokana na miradi mikubwa ya viwanda hayashangazi tena au hata kukanushwa. Kinyume chake, tukio linapotokea, huenda muelekeo ukawa ni ule wa kutafuta mradi wa viwanda ambao unaangushiwa lawama. Mnamo mwaka 2008, tetemeko la ardhi la ukubwa wa kipimo cha 8 lililikumba eneo la Ngawa, China, na kuua watu wapatao 90,000, likaharibu zaidi ya miji 100, na kubomoa nyumba, barabara na madaraja. Kwa haraka, tahadhari iligeukia kwenye Bwawa la Zipingpu lililo karibu, ambalo hifadhi yake ilikuwa imejazwa maji miezi michache iliyopita…"[1]

Mara nyingi watu huyaita majanga ya asili kuwa ni 'matendo ya Mungu', lakini kwa kweli, maafa zaidi na zaidi yanatokea kutokana na shughuli za kibinadamu. Kwa kushangaza, badala ya kuwa ni matendo ya Mungu, majanga yote ni matokeo ya uasi wa mwanadamu dhidi ya Mungu. Kwani kama tulivyoona, ilikuwa ni mafuriko ambayo yalisababisha hali hizi hapo mwanzoni. Na nini kilisababisha mafuriko?

Mwanzo 6:5 BWANA akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote.
6:6 BWANA akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo.

Uovu wa mwanadamu wakati wa Nuhu ulikuwa ni mwingi sana kiasi kwamba kwa ajili ya vizazi vijavyo, Mungu alilazimika kuwaangamiza. Hata hivyo, ni lazima isemwe, kwamba Mungu aliwaongezea wale waliopita kabla ya gharika miaka 120 ya rehema ili watubu dhambi zao na kutafuta kimbilio ndani ya safina. Lakini kwa sababu ya upendo kwa

1 Gillian Foulger, Jon Gluyas and Miles Wilson, "California's Rain May Shed Light On New Questions About What Causes Earthquakes," The Conversation, February 24, 2017. https://theconversation.com/californias-rain-may-shed-light-on-new-questions-about-what-causes-earthquakes-73571.

wanadamu, uasi wa mwanadamu ulipaswa kufikia ukomo. Hukumu ilipaswa kupatikana ili kuwakomboa wanadamu.

Hatimaye, uovu wote kwenye ulimwengu huu, maumivu yote na ukosefu wa haki, ni matokeo ya uasi wa mwanadamu dhidi ya Mungu. Sasa kwa kuwa tunajua sababu ya kuteseka, tunaweza kuelewa kwa urahisi zaidi ni kwa nini Mungu anaruhusu kuteseka kuendelee. Unaona, ili Mungu afikishe ukomo wa kuteseka—na Atafanya hivyo—ni lazima afikishe ukomo wa dhambi. Hii ina maana ya kuweka ukomo wa wenye dhambi, ambayo ina maana kwamba watu wengi ulimwenguni watapotea.

Sasa, wengi wanaweza kudai kuwa wao si watu wabaya. Nimewajua watu wengi ambao kwa kadri ya viwango vya kijamii, hakika ni watu wazuri. Lakini kama tulivyoona kwenye kitabu cha Yakobo, ingawa mtu haibi au kufanya uzinzi, hiyo haimaanishi kwamba havunji sheria ya Mungu. Angalia ni nani mwingine alijiona kuwa hatalaumiwa kwa mujibu wa sheria. Maandiko yafuatayo yanatoka kwa mtume Paulo, akizungumzia maisha yake ya zamani kama Sauli wa Tarso.

> Wafilipi 3:6 kwa habari ya juhudi, mwenye kuliudhi Kanisa, kwa habari ya haki ipatikanayo kwa sheria, sikuwa na hatia.

Sauli alifikiri kuwa hatalaumiwa, na bado alikuwa akiwatesa na kuwaua Wakristo wasio na hatia. Amri zinazama ndani zaidi na ni za mbali kuliko vile tunavyofikiri. Yesu alifundisha kwamba hata kama mtu hataua au kufanya uzinzi, kwa kuwa na hasira tu au kumuangalia mwanamke kwa matamanio, basi anakuwa na hatia ya dhambi. Hisia hizi za tamaa na hasira zinatokana na mawazo ya mtu. Kwa hiyo, amri zinahukumu sana mawazo ya mtu, na si tu matendo ya kimwili.

Amri ya kumi—usitamani—kwa kweli ni mzizi wa dhambi zote, na hufanyika kwenye akili. Kwa mfano, mwanaume anafanya uzinzi kwa sababu anamtamani mwanamke mwingine. Mtu anaiba kwa sababu anatamani kitu ambacho si chake. Lusifa alikitamani kiti cha enzi cha Mungu, na dhambi hiyo ndiyo iliyosababisha vita mbinguni na kupelekea hali tuliyonayo leo hii. Kwa hivyo, amri ya 'usitamani' inapenya

kwenye amri zote kumi. Hii inaiweka ndani ile amri ya kwanza, inayotuagiza kwamba tusiwe na miungu mingine isipokuwa Mungu wa kweli, ambaye tunapaswa kumpenda kwa moyo wetu wote, nafsi na akili zetu zote. Tunapotamani vitu vingine zaidi ya Mungu, tunakuwa na hatia ya dhambi. Tabia nyingine mbaya kama vile husuda na wivu ni matokeo ya kutamani. Kiuhalisia, kutamani ni tabia ambayo kila mtu anapaswa kupingana nayo kwa kiwango kikubwa au kidogo. Ni kwa uwezo wa Kristo pekee ndipo unaweza kuushinda muelekeo huu mbaya. Kwa kweli, wivu na kutamani vilikuwa ni sababu ya moja kwa moja ya kifo cha Yesu. Viongozi wa Kiyahudi walikuwa na wivu kwa Kristo. Walihusudu umaarufu Wake kwa watu, uwezo wa mafundisho Yake, na miujiza Aliyoifanya. Angalia Biblia inachosema kuhusu Pontio Pilato wakati viongozi wa Kiyahudi walipompeleka Kristo ili akasulubiwe.

> Mathayo 27:18 Kwa maana alijua ya kuwa wamemtoa kwa husuda.

> Marko 15:10 Kwa maana alitambua ya kuwa wakuu wa makuhani wamemtoa kwa husuda.

Mtu pekee asiye na hatia aliyepata kuishi alisulubishwa kwa sababu ya wivu. Kama ambavyo huu mstari ufuatao unavyoonesha, ulikuwa ni wivu ambao pia ulisababisha kuuawa kwa Paulo.

Matendo ya Mitume 13:45 Bali Wayahudi, walipowaona makutano, wakajaa wivu, wakakanusha maneno yaliyonenwa na Paulo, wakibisha na kutukana.

Tunahitaji kutambua kuwa matendo yetu mabaya—dhambi zetu—husababisha mateso. Zaidi ya hayo, mateso hayapo kwenye ulimwengu huu tu. Sisi ni wanadamu tuliopotoka, lakini tunapotazama habari na kushuhudia majanga yanayotokea, tunateseka. Inatuumiza kuona matokeo ya majanga ya asili, kushuhudia umaskini, au kusikia watu wasio na hatia wakitendewa vibaya. Je, unadhani Mungu anateseka zaidi kiasi gani? Sisi ni wanadamu tuliopotoka, lakini Mungu ni mtakatifu. Na kadri unavyokuwa mtakatifu na mkamilifu zaidi, ndivyo unavyouhisi zaidi uovu. Wale ambao wamezoea sana uhalifu, na ambao

dhamira zao zimekaribia kunyamazishwa kabisa, hawayasikii sana majanga. Hata hivyo, Mungu wetu mkamilifu na mtakatifu anashuhudia kila ukosefu wa haki unaotendeka. Anaona kila mtoto anayelia kwa uchungu na njaa. Anatazama matukio haya kila dakika ya kila siku. Unafikiri Anajisikiaje? Je, unafikiri Mungu anataka kuruhusu mateso hayo yaendelee? Mungu haangalii tu matukio ya ulimwengu huu; Anaumizwa nayo. Angalia Yakobo anasema nini kuhusu maskini na waliokandamizwa wanaomlilia Mungu:

> Yakobo 5:4 Angalieni, ujira wa wakulima waliovuna mashamba yenu, ninyi mliouzuia kwa hila, unapiga kelele, na vilio vyao waliovuna vimeingia masikioni mwa Bwana wa majeshi.
> 5:5 Mmefanya anasa katika dunia na kujifurahisha kwa tamaa; mmejilisha mioyo yenu kama siku ya machinjo.
> 5:6 Mmehukumu mwenye haki mukamwua; wala hashindani nanyi.

Mungu anaona kila tendo la ukosefu wa haki na ukatili. Siku si nyingi Atayapa ukomo. Katika Injili ya Mathayo, tunamsoma Yesu akitetea haki ya Baba yake, kama sisi tunavyopaswa kufanya. Akiwa na mtoto mapajani mwake, Alisema:

> Mathayo 18:10 Angalieni msidharau mmojawapo wadogo hawa; kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni.

Yesu alifundisha kwamba kila mtoto anaye malaika wake mbinguni ambaye anatoa taarifa ya hali yake kwa Baba. Nina uhakika kuwa hakuna hata mmoja wetu ambaye angekuwa hai leo kama isingekuwa ulinzi wa malaika. Ninaweza kushuhudia mimi binafsi kwamba hata kabla sijamjua Mungu, ilikuwa ni muujiza kwamba nimekuwa hai hivi. Ninamshukuru Mungu kwa majaaliwa yake, na ulinzi wa malaika zake na kwamba maisha yangu yalidumishwa na niliweza kufanya uamuzi wa kumfuata.

Ijapokuwa pamoja na hayo, wengine huuliza ni kwa nini Mungu anaruhusu kuteseka kana kwamba yeye Mungu hili jambo halimhu-

su, ilhali ni jambo la maana zaidi Kwake kuliko linavyoweza kutokea kwetu. Ajabu ni kwamba, mara nyingi wakosoaji na wale wasiomuamini Mungu ndio huuliza swali hili, ilhali wao wenyewe wanaiasi sheria ya Mungu. Wao wenyewe husababisha kuteseka, na wakati huo huo wanamhoji Mungu ni kwa nini anaruhusu kuendelea kwa mateso. Wana tamaa. Wana wivu. Na wanashuhudia uongo. Wao ni wepesi wa kuonesha ufisadi, umaskini, na maovu katika dunia lakini hawaoni chochote kibaya kwenye maisha yao wenyewe. Wanataka Mungu afanye jambo fulani kuhusu matatizo ya ulimwenguni, lakini hawataki Mungu afanye lolote kuhusu matatizo yao. Na wakati huo huo, wao ni sehemu ya matatizo ya ulimwengu. Lakini wanamlaumu Mwenyezi Mungu kwa kutofanya jambo lolote kuhusu hilo.

Wawili kati ya wanaume mashuhuri waliowahi kuishi ni Francois Voltaire na Thomas Paine. Maandishi yao yalihamasishwa na Shetani kuharibu Ukristo, Biblia, na uchaji wa Mungu. Wanaume hawa walikuwa na imani fulani. Waliamini katika mungu ambaye alianzisha ulimwengu huu na kisha akauacha ujitawale. Deism ni kinyume cha Calvinism, lakini wote ni waongo sana. Ingawa John Calvin alikuwa ni Mkristo, alifundisha baadhi ya makosa makubwa sana. Calvin alifundisha kuwa Mungu anaongoza kila sehemu ya maisha duniani. Alidai kwamba Mungu Amepanga kila kitu tangu hapo awali, ikiwa ni pamoja na kama mtu ataokolewa au laa. Kwa upande mwingine, Voltaire aliamini kwamba Mungu hana mchango wowote kwenye mambo ya ulimwengu huu. Hivyo, alitoa hoja kwamba Mungu ndiye mwenye kulaumiwa kwa mateso yote yanayotokea tangu alipoiumba dunia hapo mwanzoni.

Theolojia zote mbili ni za uongo. Ukweli ni kwamba mwanadamu ana hiari ya kufanya jambo. Serikali zinaweza kuchagua kupitisha sheria ambazo Mungu anaziona kuwa ni za kukufuru. Watu wanaweza kuchagua kutomtii Mungu na kutenda isivyopaswa. Na licha ya uchaguzi mbaya wa mwanadamu, bado daima Mungu anafanya kazi kulinda na kuokoa uhai. Soma Zaburi ya 34 na ya 139 kwa maelezo ya ajabu ya ulinzi na uangalizi wa Mungu. Sababu ya sisi kuwa hai leo ni Mungu anayedhibiti matukio ya ulimwengu huu. Siku si nyingi, Mungu atawaamuru malaika waziachilie zile pepo nne za ugomvi, na dunia

itatumbukizwa kwenye mzozo wenye kutisha zaidi kuliko kitu chochote ambacho kimewahi kushuhudiwa. Kwa sasa, Mungu anazizuia hizo pepo.

Nukuu ifuatayo kutoka kwa Voltaire inaangazia jitihada yake ya kuharibu Ukristo.

> “Nimechoka kusikia watu wakirudia kusema kuwa wanaume kumi na wawili walianzisha dini ya Kikristo. Nitathibitisha kwamba mtu mmoja anatosha kuipoteza.”[2]

Mnamo mwaka 1776, Voltaire alidai hivi: “Miaka mia moja ijayo Biblia itakuwa ni kitabu kilichosahauliwa.” Voltaire alikufa miaka miwili baadaye. Mnamo mwaka 2019—miaka 243 baada ya taarifa hii kutolewa—Biblia ndicho kitabu kinachosomwa zaidi, kilichochapishwa zaidi, na kinachouzwa zaidi duniani, na inakadiriwa kuwa nakala bilioni tano ziliuzwa na kusambazwa. Mwanadamu anayekufa anapaswa kutetemeka kwa mawazo ya majivuno namna hii mbele ya Muumba wa ulimwengu.

Maandishi ya Voltaire yalikuwa ni moja ya ushawishi mkuu wa Mapinduzi ya Ufaransa. Yeye na Wafaransa hawakukubali jinsi ambavyo Mungu mwenye upendo angeweza kuruhusu kuteseka, taabu, na ukosefu wa haki. Watu walijua kuhusu ufisadi wa kufedhehesha kwenye utawala wa kifalme na kwenye Kanisa Katoliki. Waliwaona mapadri wakiishi maisha ya anasa huku wananchi wakiwa na njaa. Ilikuwa sawa kwao kuyahoji mashirika hayo, lakini si kumlaumu Mungu. Wafaransa, hata hivyo, walimlaumu Mungu, na matokeo yake wakakataa kumuabudu Yeye kabisa. Kwa kweli, walimuinua mungu mpya ambaye walimuita mungu wa kike wa kuhoji. Waliisimamisha sanamu ya mungu huyu wa kike—kahaba—kuonesha kuwa akili ya mwanadamu ilikuwa ni kubwa kuliko ya Mungu. Dhana hii inaenea kupitia maandishi ya Voltaire na Paine.

---

2 William Patrick Palmer, A Compendious Ecclesiastical History, (London: James Burns, 1840), 239-240.

Zawadi yao ilikuwa ni nini? Kwenye kumuacha Mungu wa Biblia, Ufaransa ilipokea kile kinachojulikana kama utawala wa ugaidi. Utawala wa ugaidi ulidumu kwa miaka kumi na uliashiria moja ya nyakati mbaya zaidi katika historia ya ulimwengu huu. Ufisadi, ukatili, matatizo, na uasherati uliendelea, na ulikuwa mbaya kwa kiwango cha mara mia zaidi. Watu walipoteza mali zao na maisha yao bila sababu yoyote. Ilikuwa ni kipindi cha machafuko kamili na ya jumla. Kile ambacho kilipaswa kuwa miaka ya kuelimika kilikuwa kimegeuzwa kuwa miaka ya misukosuko na vita.

Unaona, wakati Mungu na sheria yake inashutumiwa, uovu ni matokeo yasiyoepukika. Hakuna kitu kizuri kinachoweza kutoka kwa kuacha sheria ya Mungu. Mungu alitangaza jambo hili kupitia nabii Hosea.

> Hosea 4:1 ...Bwana ana mateto nao wakaao katika nchi, kwa sababu hapana kweli, wala fadhili, wala kumjua Mungu katika nchi. 4:2 kuapa kwa uongo, na kuvunja ahadi, na kuua, na kuiba, na kuzini; huruka mpaka, na damu hugusana na damu.
>
> 4:6 Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; ...kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako...

Kumcha Mungu inapokataliwa, kama ilivyokuwa wakati wa Mapinduzi ya Ufaransa, matokeo yote ni “kuapa, na kusema uongo, na kuua, na kuiba, na kuzini; huruka mpaka, na damu hugusana na damu.” Mapinduzi ya Ufaransa yalikuwa onesho la matokeo ya kumkataa Mungu na sheria yake. Katika tukio hili la kihistoria, onyo la Hosea lilijionesha.

Zaidi ya hayo, ili kuelewa masuala haya kwa usahihi, mtu anapaswa kuyatazama kwa mwanga wa kitu kinachoitwa pambano kuu. Pambano hilo kuu lilianzia mbinguni wakati Shetani alipoishawishi theluthi moja ya malaika wa mbinguni ili waiasi serikali ya Mungu. Hii ilisababisha kufukuzwa kwa Shetani na wafuasi wake kutoka mbinguni. Mara tu Shetani alipomfanya Adamu atende dhambi, pambano hili liliingia kwenye familia ya wanadamu, na limeendelea duniani mpaka leo hii. Hata sasa, nguvu zisizo za kawaida zinapigania maisha yako. Mungu hufanya kazi kwa uangalifu, kwa kukuchochea, na kuzungumza na

dhamira yako, ilhali Shetani anaijaza akili yako kwa majaribu ya kutisha, akitumaini kukuongoza wewe na watoto wako kwenda kwenye uovu wa kutisha. Kila wakati vita hivi vinaendelea. Lakini si Mungu wala Shetani anayeweza kulazimisha hiari ya kutenda. Ona jinsi Paulo anavyoelezea vita hivi katika barua yake kwa Waefeso.

> Waefeso 6:11 Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani.
> 6:12 Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.

Biblia—upanga wa Rohoni—ndiyo silaha kuu inayohitajika ili kupinga hila za shetani. Kitu kile kile ambacho Voltaire na Paine walidai kingekuwa ni kitabu kilichosahaulika ni ulinzi na ulinzi mkuu wa mwanadamu. Sababu kuwa, kwa nini Biblia ni ya lazima, ni kwa sababu adui yako si mtu mwingine ambaye amefanyiwa jambo baya na wewe. Wewe haupigani na nyama na damu bali, "pepo wabaya katika ulimwengu wa roho". Na unahitaji upanga wa Rohoni ili kupigana vita hivi vya kiroho.

Ni nani aliyekuwa chachu ya maandishi ya Voltaire? Ni nani alikuwa nyuma ya Mapinduzi ya Ufaransa na utawala wa ugaidi? Ilikuwa ni Shetani. Kinyume chake, ni nani aliyeongoza Marekebisho ya Kiprotestanti na kutafsiriwa kwa Biblia kwenye lugha mama ya kawaida kabisa? Ilikuwa ni Mungu. Huu ni ugomvi mkubwa uliopo. Shetani anajua kwamba endapo anaweza kuwafanya watu wasitegemee Neno la Mungu, wao hawana msaada na wanalazimika kufanya maovu. Basi wanaume na wanawake watakuwa chini ya utawala wa Shetani. Utawala wa ugaidi ni uthibitisho wa ukweli huu. Zaidi ya hayo, Shetani anajua vyema nguvu za Biblia kwa sababu Amekuwa akizishuhudia kwa miaka elfu sita. Ameona kwamba watu wanapoliamini na kulitii Neno la Mungu, maisha yanabadilishwa ambayo yeye hana uwezo nayo. Kwa hiyo, Shetani anafanya kazi bila kuchoka kuiharibu imani kwenye Biblia.

Voltaire alipokufa, Shetani alipata mtu mwingine ili kuendeleza kazi hiyo. Jina la mtu huyo lilikuwa ni Thomas Paine. Kauli zinazofuata zina-

chukuliwa kutoka kwenye kitabu cha Paine, *The Age of Reason*.

> "Ni kutoka kwenye Biblia ambapo mwanadamu amejifunzia ukatili, ubakaji, na mauaji; kwa maana imani ya Mungu aliye katili humfanya mtu awe ni mkatili."[3]

> "Kwa ujumla, watu hawajui ni uovu gani uliomo kwenye neno hili la Mungu la kujifanyisha... ni kitabu cha uongo, uovu, na kufuru."[4]

Nikiwa kama Mkristo na nikasoma nukuu hizi ninajawa na hofu. Hata hivyo kitabu hiki kimehamasisha mamilioni ya watu. Bila shaka, tunajua ni nani aliyekuwa nyuma yake. Na ilikuwa ni kwa sababu Voltaire na Paine hawakuelewa jinsi ambavyo Mungu mwenye upendo angeweza kuruhusu maumivu na kuteseka mpaka wakaandika hivi. Kwa kusema hivyo, wanaume hawa pia waliandika mambo mazuri, ambayo ni sehemu ya sababu ya kuendelea kuwa na ushawishi huo. Walitetea haki ya binadamu ya uhuru wa kusema na uhuru wa kiimani na dhamira. Na walitumia haki hizi vizuri kwenye kuelekeza ukosoaji kwenye utawala mbovu wa kifalme na dini iliyopangwa wakati huo. Hata hivyo, hatimaye, wanaume hawa walitumia mawazo na maandishi yao kuishambulia Biblia na Mungu wa Biblia, na kuwaongoza watu kuwa waasi na wasioamini. Cha kushangaza, unaposababisha mtu kupoteza imani kwenye Biblia—kwa sababu unapinga maovu ya jamii—unachangia maovu kwenye jamii. Kwa maana kitu pekee kinachoweza kumzuia mtu asifanye mabaya ni Mungu. Ni Roho wa Mungu anayemtia moyo na kumtia nguvu mtu kukataa jambo lililo baya na kufanya jambo lililo sawa. Unaposababisha mtu akose imani kwenye Biblia kwa sababu ya kuhangaikia ukandamizaji na mateso yanayotokea ulimwenguni, unaongeza tu uonevu na mateso hayo. Hivi ndivyo ambavyo Shetani amewadanganya watu.

Unaona, mtu anapoanza kuitii Biblia na kuishi kulingana na maagizo yake, anawacha kufanya dhambi. Anawacha kuwa mbinafsi na kuwao-

---

3 Thomas Paine, The Age Of Reason: Being An Investigation Of True And Fabulous Theology, (New York, London: G.P. Putnam's sons, 1896), 198.
4 Ibid, 103.

nea wivu watu wengine. Anakuwa baba mwenye upendo na mume muaminifu. Anaijali jamii na kuwa baraka kwenye sehemu yake ya kazi na jamii. Licha ya jambo hili, wanaume kama vile Voltaire na Paine wangekufanya upoteze imani kwenye Maandiko. Na hoja zao bado zinatengeneza waasi mpaka leo hii, mamia ya miaka baada ya vifo vyao.

Charles Templeton, kama ilivyotajwa hapo awali, alikuwa ni muinjilisti Mkristo aliyeiacha imani yake. Dondoo ya habari hapa chini inaonesha kitabu alichokuwa akikisoma wakati wa kifo chake.

> "Mnamo mwaka 1946, Chama cha Taifa cha Wainjilisti kilimtaja Templeton kama "mtu anayetumiwa vyema zaidi na Mungu" na kuchukua nafasi ya Billy Graham. Hata hivyo, Chuck alikuwa na mashaka makubwa juu ya uhalali wa Biblia na mashaka hayo yaliongezeka alipokuwa akisoma kazi zisizo maarufu za wakosoaji maarufu. Aliandika kwenye Charles Templeton: An Anecdotal Memoir, "Nilikichukua kitabu cha The Age of Reason cha Thomas Paine. Baada ya masaa machache, karibia kila kitu nilichokijua au kukiamini kuhusu dini ya Kikristo kilipingwa na kwa sehemu kubwa kuharibiwa." Siku kumi zilizofuata, alisoma kitabu cha Francois Voltaire cha The Bible Explained at Last…sasa Chuck alikuwa akitilia shaka imani yake na kuyaamini mashaka yake!"[5]

Bado hadi leo, vitabu hivi vinasababisha watu wakose imani na Mungu. Hata awapo kaburini, mtu anaweza kuwa na pumzi ya uzima iendayo uzimani au ya kifo mpaka kifo. 2 Wakorintho 2:16. Wanaume hawa walitetea uhuru wao wa kujieleza, wakati kiukweli, hawakuwa huru hata kidogo. Walikuwa watumwa wa bwana wa kawaida. Mtume Paulo alisema:

> Warumi 6:16 Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa

---

5 Don Boys, "Pathetic Preacher Dies in Unbelief!," CST News, Aug 8, 2005. http://www.cstnews.com/bm/other-hot-topics-for-informed-christians-cstnews/pathetic-preacher-dies-in-unbelief.shtml.

> wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki?

Pambano kuu sio tu linaendeshwa kati ya viumbe watakatifu na wale waovu. Linaendeshwa akilini mwako. Hapo ndipo vita inapiganiwa. Je, utamtii nani pale dhamira yako inapozungumza na wewe? Fikiria kipindi cha nyuma ulivyokuwa mtoto na ujaribu kukumbuka hatia ambayo ungeihisi wakati ulipofanya kitu kibaya. Hiyo ilitokea wapi? Ilikuwa ni sauti ya Mungu ikishindana nawe huku Shetani akikujaribu utende dhambi. Ukweli ni kwamba, ama unamtii Shetani, na unakuwa mtumishi wake hadi kufa, au unamtii Mungu, na wewe kuwa ni mtumishi wake kwenye haki, ambapo mwisho wake ni uzima wa milele.

Voltaire na Paine walijivunia uhuru wao wa kujieleza, hata hivyo walikuwa ni watumishi wa Shetani, wakiwaongoza watu kuingia kwenye dhambi na hatimaye kuzimu. Hakika watavuna walichokipanda. Petro anasema jambo kama hilo anapozungumza kuhusu viongozi wa kidini wa enzi hizo ambao walikuwa ni wale waliokengeuka.

> 2 Petro 2:19 Wakiwaahidia uhuru, nao wenyewe ni watumwa wa uharibifu, maana mtu akishindwa na mtu huwa mtumwa wa mtu yule.

Watu hawa ambao Petro anazungumza juu yao walikuwa ni wale waliokengeuka, na bado walifikiri kuwa wangeweza kuhubiri uhuru kwa watu wengine. Walikuwa kwenye utumwa wa asili zao za ubinafsi na Shetani aliwadhibiti na kuwatumia vile ambavyo yeye angetaka. Kumbuka onyo la Yesu kwa Petro: “Simoni, Simoni, tazama, Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; Lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike.” Luka 22:31-32.

Rafiki zangu, hamuwezi kutenganisha mateso na dhambi. Dhambi ndiyo sababu ya kuteseka, na Yesu atakapokuja ataweka ukomo wa dhambi. Atawapa ukomo wale wenye dhambi na hakutakuwa na mateso tena. Lakini kama Yesu angerudi leo hii, maelfu wangepotea ambao wangeweza kuokolewa kama Kristo angekuja kesho au juma lijalo. Wanadamu wanashangaa ni kwa nini Mungu anaruhusu kutese-

ka na bado ni kwa rehema zake kuu kwamba Mungu anaruhusu uzima uendelee kwa sababu anataka kuokoa roho yako. Anataka kukupatia uzima wa milele. Mungu aliupa ulimwengu wa kabla ya gharika muda wa miaka 120 ili utubu dhambi na kutafuta kimbilio ndani ya safina. Hata hivyo, baada ya muda huo, gharika ilikuja. Mungu ni mwenye rehema na mvumilivu, lakini hatasitasita milele. Angalia Mungu anasema nini kwenye kitabu cha Ezekieli wakati wana wa Israeli walipokuwa wakipotea.

> Ezekieli 18:32 Kwa maana mimi sikufurahii kufa kwake afaye, asema Bwana MUNGU; basi ghairini, mkaishi.

> Ezekieli 33:11 Waambie, Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu; bali aghairi mtu mwovu, na kuiacha njia yake mbaya, akaishi. Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa, Enyi nyumba ya Israeli?

Ninakipenda kifungu hiki kwa sababu kinaangazia utu wa Mungu kama Baba yetu. Inaonesha Mungu akitusihi kubadilika kama vile tunavyowasihi watoto wetu pale tunapowaona wakifuata njia zenye uovu. Mungu hafurahii mateso au kifo cha waovu. Yeye huwapigania wanadamu kila siku; akiwasihi waache njia zao mbaya ili waokolewe. Kwa ajili yako anairuhusu dunia kuendelea kuwepo kwa muda mrefu zaidi. Anayahifadhi maisha yako kwa matumaini kwamba utayasikia maombi yake, na anaweza kukuokoa milele.

Yesu alifundisha kwamba Msaidizi atakapokuja, "atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu." Yohana 16:8. Ahadi hii inatimizwa kila wakati unapojisikia hatia kwa kufanya kitu kibaya, na vile vile kila wakati unapokuwa na mawazo mazuri, msukumo wa upendo, au nia iliyo safi. Wakati mtu anapofikiria juu ya mbingu na uzima wa milele, hiyo haitokei kwa bahati mbaya tu. Msukumo huo unatoka kwa Yule ambaye "amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu," Yohana 1:9. Ni Mungu anayeufurahisha moyo wako na kusema na dhamira yako. Usipoipinga sauti hiyo, Mungu ataendelea kukuvuta, na atayabadilisha maisha yako sasa na hata milele.

Ni kweli kwamba Mungu anataka kuweka ukomo wa mateso, lakini pia anataka kukuokoa. Na kwa hivyo Halali wala Hasinzii. Mbingu inampigania kila mtu. Kwenye kitabu cha Tito 2:11 tunaahidiwa: "Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa;" wengine wanauliza kuhusu wale ambao hawajawahi kuisikia injili. Wanashangaa jinsi ambavyo Mungu anavyowahukumu wale walio kwenye maeneo ya mbali ambao hawajapata hata kuisikia Biblia. Ukweli ni kwamba hata kwenye sehemu za mbali sana na miongoni mwa watu wapagani zaidi, bado kuna ujuzi wa mema na mabaya. Dhamira zao wenyewe huwaambia kuwa ni kosa kuua, kusema uongo, na kufanya uzinzi. Ujuzi huo ulitoka wapi? Ulitoka kwenye neema ya Mungu ambayo imeonekana kwa watu wote. Na neema hiyo inatufundisha nini? Mstari unaofuata unafunua kuwa neema ya Mungu "Nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa;" Tito 2:12.

Neema hii inaonekana kwa kila mwanadamu mpaka pale utakapompinga kabisa Roho wa Mungu na kukataa kuisikia sauti yake tena. Hata hivyo, ikiwa watu wangeisikiliza sauti hiyo ikizungumza na dhamira zao, na wasiipinge, maisha yao yangebadilishwa upesi sana. Kwenye kitabu cha Yohana 1:12 tunasoma: "Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake;" Unapompokea Kristo maishani mwako, unapokea pia nguvu za Kiuungu za kuzishinda dhambi.

Hatimaye, kuna njia mbili ambazo mtu anaweza kuzifuata. Anaweza kuuitikia mvuto wa Mungu na kushika uhakikisho huo uliobarikiwa wa uzima wa milele, au anaweza kuwa mgumu zaidi na zaidi kwa kumpinga Roho Wake, na kufuata njia inayomuongoza kwenye dhambi na kifo. Kwa maana kama tulivyoona hapo awali, "ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake." Warumi 6:16. Kuna nguvu zinazopigania nafsi yako. Kwa kuzingatia hili, unaweza kufanya maamuzi sahihi zaidi. Kwa kuchagua kumtii Mungu, hautaacha tu kuwapa wengine mateso moja kwa moja, bali pia utasaidia kuharakisha ujio wa Bwana ili Aweze kuweka ukomo wa kuteseka. Kinyume chake, endapo unapuuza sauti ya Mungu, utaendelea tu kuongeza dhambi na mateso kwenye ulimwengu huu. Kwa mfano,

mwanaume anaweza kufurahia maisha ya familia yenye furaha na bado akavutwa kuingia kwenye kucheza kamari. Tabia hiyo ya kucheza kamari ikimshinda, anaweza kujiharibia yeye mwenyewe na pia familia yake. Hali kama hizi hutokea kila wakati.

Hapa kuna kielelezo kingine kinachofunua mahali ambapo mateso yanatokea, na jinsi ambavyo hayana uhusiano wowote na Mungu. Hebu fikiria jiji lenye sifa zake zote za kawaida; kituo cha polisi, mahakama, vituo vya kulea wazee, na magereza. Hebu fikiria kuwa kuanzia kesho na kuendelea, kila mwananchi kwenye mji huo anaamua kutotenda dhambi. Mzinzi anaamua kuwa hatazini tena. Mwizi anaamua kuwa hataiba tena. Watoto kuamua kuwaheshimu wazazi wao. Kila amri inafuatwa vyema kabisa. Ni nini kinatokea kwenye jiji kama hilo? Ni wazi kwamba uovu, ufisadi, ukosefu wa heshima, na chuki hutoweka. Ni kweli kwamba hakutakuwa tena na uhitaji wa jeshi la polisi, mahakama, vituo vya kuwatunzia wazee, au magereza. Hakuna wahalifu wa kuwakamata. Hakuna wa kumpeleka kwa hakimu. Na watu wanawatunza wazazi wao ambao ni wazee. Bila Mungu kuingilia, visababishi vikuu vya kuteseka vyote hutoweka. Ingawa jambo hili kamwe halitatokea kwenye maisha halisi, kielelezo hiki kinaonesha jinsi ambavyo wingi wa mateso hufikia ukomo wakati wanadamu wanapoanza kumtii Mungu badala ya kutomtii. Kando na suala la kuvuna matokeo ya dhambi zilizopita, na uozo usioepukika wa afya na uzee, hiki ndicho kinachotokea wakati wanadamu wanapoanza kuisikiliza sauti ya Mungu, na kuishi kwa kiasi, haki, na kumcha Mungu kwenye ulimwengu huu wa sasa.

Marafiki zangu, mnao uwezo wa kufanya maamuzi haya. Siku zote dhambi ni chaguo. Kamwe haiepukiki. Ni kweli kuwa unauhitaji msaada wa Mungu, lakini una uwezo wa kusema hapana. Wengi wanafikiri kwamba wana tabia ambazo hawawezi kuziacha. Hata hivyo, fikiria kielelezo kifuatacho cha mtu anayeonekana kuwa mtumwa wa dhambi fulani. Hebu fikiria kwamba mtu huyu amefungiwa kifaa cha umeme na kila anapochagua kufanya dhambi hiyo, anapigwa na mamia ya shoti za umeme. Je, unadhani ni mara ngapi zaidi angetenda dhambi hiyo? Ninathubutu kusema hatofanya dhambi hiyo hata mara moja! Mtu huyo angebadilishwa haraka sana. Hiyo ndiyo nguvu ya matakwa

ya mwanadamu. Hadithi za wafungwa wa vitani, na wale waliopotea kwenye maeneo ya mbali hukazia suala la umbali ambao wanadamu wataenda ili kujiokoa na kuweza kuishi. Matakwa ya mwanadamu yana nguvu sana. Na unapoyaweka mikononi mwa Mungu, unaweza kuishinda kila tabia mbaya na maisha yako yanaweza kubadilishwa.

Katika mfano wa jiji hilo, kulikuwa na upatano na amani wakati wanadamu walipoacha kutenda dhambi. Hivyo ndivyo mbingu zitakavyokuwa. Ninachotazamia zaidi mbinguni si mitaa yenye dhahabu au utukufu na maajabu makubwa. Sio mambo ambayo Yesu anasema: "jicho halijaona, wala sikio lililosikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu amewaandalia wampendao." Ninachotazamia zaidi ni kujua kwamba unaweza kuwa na mazungumzo na mtu kama Musa au Paulo, na bado hawatakudharau kama mtu asiyestahili kuwa pamoja nao. Hakutakuwa na vitisho au hisia za mtu fulani kuwa ndiye bora zaidi ya mwingine. Utakaa pamoja na Yesu, Muumba wa ulimwengu, na kujisikia vizuri kabisa kwenye uwepo Wake. Badala ya mipaka, kutakuwa na upendo kamili na heshima kwa kila mmoja. Hivyo ndivyo Mungu alivyotamani iwe kwenye ulimwengu huu, na jinsi ambavyo jamii ingeweza kuwa kama watu wangebadili njia zao na kutii sauti ya Mungu. Ufunuo 22:14 inaeleza aina ya watu wanaokwenda kuwepo mbinguni.

> Ufunuo 22:14 Heri wazitendao amri zake, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake.

Ni dhambi iliyoondoa haki ya mwanadamu kwenye mti wa uzima. Wanadamu wanapoacha kutenda dhambi na kuchagua kumtii Mungu, wanapata haki hii tena. Kiingilio kwenye mji wa mbinguni kitatolewa tu kwa wale wanaozishika amri za Mungu. Kisha, hali bora ya Mungu kwa familia ya kibinadamu itatimizwa, na watoto Wake watiifu na wasio na ubinafsi wataifurahia raha na amani isiyoelezeka milele. Hata hivyo, ili hilo litokee, ni lazima Mungu aruhusu kuendelea kuteseka kwa muda fulani hapa duniani. Unaona, kila mtu anayeingia kwenye malango ya mbinguni aliwahi kuwa ni mtu mwenye dhambi. Kila mtu alihusika kwa sehemu kusababisha mateso kwa wengine. Lakini kwa rehema na ustahimilivu wa Mungu, aliwaweka hai. Kisha siku moja waliitikia

neema ile iletayo wokovu, na Mungu akawapa wao uzima wa milele.

Kando na Yesu, mtu mwenye hekima zaidi aliyepata kuishi alikuwa ni Mfalme Sulemani. Biblia inasema kwamba Mungu alimpa hekima ambayo hakuna mwanadamu, kabla au baada yake, angeweza kuwa nayo. Sulemani aliandika mamia ya mithali pamoja na kitabu cha Mhubiri. Sulemani alipokuwa mzee akihubiri, alitazama uzoefu wake wa maisha na hekima yote ambayo Mungu alimpatia, na akafupisha kusudi la maisha kwenye mstari huu mmoja:

> Mhubiri 12:13 Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike amri zake. Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu.
> 12:14 Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya.

Hii ndiyo hekima yenye thamani na yenye kupendeza zaidi ambayo mtu anaweza kuipata. Kitu chochote nje ya shauri hili—falsafa zote za ulimwengu—ni ujinga mtupu na ubatili tu. Rafiki zangu, Mungu hana upendeleo. Bila kujali wewe ni tajiri au maskini, maarufu au haujulikani, Mungu anaona makundi mawili tu: waliookolewa na waliopotea. Mungu huwaona wale wanaoshika amri zake, na wale wasiofanya yanayotakiwa. Na Mungu si mjinga wa mambo yanayotokea hapa duniani. Atatoa hukumu ya kila kitu kilichopo, na haki itapatikana siku si nyingi.

Hakika kuna hekima nyingi kwenye kifungu hiki. Aya hii moja ina jibu la matatizo yote ya wanadamu. Ikiwa tungezishika amri za Mungu, kusingekuwa na dhambi tena na kwa sababu hiyo, hakutakuwa tena na dhuluma, ufisadi, uovu au ukosefu wa uaminifu. Kwa kawaida, mateso yote ambayo dhambi hizi huleta yangefikia ukomo kwa haraka.

Bila shaka, hakuna mtu anayependa kuteseka. Hata hivyo, kuteseka ni sehemu ya maisha ya mwanadamu. Ulimwengu huu umepotoshwa, asili zetu zimepotoshwa, na mateso ni sehemu ya maisha ya duniani. Na mateso hayabagui. Unaweza kuwa tajiri na kufanikiwa na bado kwa wakati fulani ukapokea simu ya taarifa ya kifo cha mpendwa wako na ikayaharibu mazuri yako yote.

Kuna sababu nyingine inayomfanya Mungu aruhusu majaribu na mambo magumu yatupate. Yesu aliahidi hivi: "Ulimwenguni mnayo dhiki; Lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu." Yohana 16:33. Ukweli ni kwamba utateseka kwenye ulimwengu huu, iwe kwa ajili ya injili au kutokana na matokeo ya dhambi zako. Je, isingekuwa bora zaidi kuteseka kwa ajili ya Kristo na kuthamini tumaini la uzima wa milele wenye baraka ambao unakuja? Wale wanaomkataa Mungu na kuendelea na dhambi bado wataendelea kuteseka kwenye ulimwengu huu, lakini pia watapata adhabu ya kifo cha milele. Petro na mitume walipokamatwa na kupigwa bila ya kutendewa haki, Biblia inasema kwamba "nao wakatoka katika ile baraza, wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo." Matendo ya Mitume 5:41. Aidha, mateso na magumu yanaweza kuwa ni mambo yenye manufaa kwetu. Angalia hekima ya Mungu kwenye kuilaani ardhi kwa ajili ya mwanadamu baada ya Adamu kufanya dhambi.

> Mwanzo 3:17 Akamwambia Adamu, Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikasema, Usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako;
> 3:18 Michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni;
> 3:19 kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.

Mungu Alitangaza kwamba baada ya mwanguko, maisha ya mwanadamu yangejumuisha huzuni, shida na taabu. Mambo haya yote yalikuwepo "kwa ajili yako", au kwa maneno mengine, kwa manufaa yako. Hatimaye, Mungu anamuambia Adamu kuwa atalazimika kufanya kazi kwa bidii na kuvumilia majaribu, kisha siku moja atakufa. Baada ya Adamu kutenda dhambi, asili ya mwanadamu ikawa ni ya dhambi na ya ubinafsi. Je, unaweza kuwaza juu ya jambo ambalo lingetokea endapo kila kitu kinachomzunguka kingeendelea kuwa ni kamilifu, kama ilivyokuwa kabla hajatenda dhambi? Kitu pekee kinachomzuia mwanadamu kufanya nusu ya maovu anayotaka kufanya ni ufahamu

wa matokeo yake. Mwanadamu mwenye dhambi anayeishi kwenye mazingira yaliyo kamili angeendeleza tu uovu kwa sababu hakungekuwa na madhara yoyote. Lakini mtu anapolazimika kufanya kazi kwenye ardhi, na kushughulika na miiba na michongoma, anakumbushwa juu ya kutotii amri kulikosababisha hali hiyo, na ahadi ya maisha ambayo ni kamilifu, na maisha mapya yajayo. Ni kwa sababu hii majaribu na dhiki zinaweza kuwepo kwa faida yetu.

Je, umewahi kugundua kuwa ni vigumu zaidi kumshirikisha injili mtu ambaye ni tajiri kuliko maskini au watu wa tabaka la kati? Mara nyingi wale ambao ni wagonjwa, waliotengwa, au waliokandamizwa wapo tayari zaidi kusikiliza. Kwenye magumu yao na hali zisizo na matumaini, Mungu anaweza kuwafikia kwa tumaini kwamba maisha yao hayo si ya milele, na jambo bora zaidi linawangojea. Kwa wale walio na shida, ni hali yao yenyewe inayofanya tumaini hili la injili kuwa ni ukweli kwao. Wana uhitaji, na uhitaji huo huleta tumaini. Tumaini nje ya gereza, mbali na kitanda cha hospitalini, na mbali na mizigo ya maisha haya. Ni kwa sababu ya shida na huzuni ndio maana watu huvutiwa kuisikia habari njema ya wokovu na uzima wa milele.

Pia, mwanadamu amepewa mambo kadha wa kadha kama vile imani, subira na kutosheka. Wakati mtu akiwa na imani, inamsaidia kutofadhaika au kuwa na wasiwasi. Mtu anapokuwa na subira, humzuia asikasirike na kumsaidia awe mtulivu. Na kuridhika ni kitu bora zaidi ya vyote. Ninaamini kuwa kuridhika ndiyo siri ya Mkristo wa kweli. Unaporidhika, kamwe hautatamani kitu kingine au cha mtu mwingine. Kamwe hautakuwa na wivu au husuda. Utakuwa na amani na furaha bila kujali hali yako. Na Mungu Ametupatia mfano kamili wa jambo hili ili tufuate. Kwa maana hakuna mtu aliyewahi kuishi ambaye alikuwa na imani kamilifu zaidi, au alikuwa mvumilivu zaidi kuliko Yesu. Wakati huo huo, hakuna mwanadamu aliyewahi kuishi ambaye alipitia magumu, majaribu au mateso zaidi ya Yesu. Mwokozi wetu alizungukwa na maadui. Hakuwa na makao ya kudumu ya kujilaza, na aliachwa na wanafunzi Wake kwenye nyakati ambazo aliwahitaji mno. Lakini kwenye haya yote, Yesu aliridhika. Mtume Paulo aliielewa kanuni hii, na kuitumia kwenye maisha yake yeye mwenyewe. Alikiri wazi:

> Wafilipi 4:11 Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji; maana nimejifunza kuwa radhi na hali yoyote niliyo nayo.
> 4:12 Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yoyote na katika mambo yoyote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa. 4:13 Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.

Ilikuwa ni kupitia majaribu ambapo Paulo alijifunza kuridhika. Kwa nini tunatilia shaka hekima ya Mungu? Kwa nini hatumuamini Yeye zaidi hata kidogo? Yeye ndiye Muumba wetu. Kwa kweli, ni uzoefu huu wa kujaribiwa ambao hutuwezesha kukuza uaminifu.

Baada ya kuanguka kwa soko la hisa nyakati za mtikisiko mkubwa wa kiuchumi, watu wengi wenye nguvu zaidi, matajiri waliona utajiri wao ukitoweka na kwa sababu hiyo, walijiua. Watu hawa walikuwa wamezitumainia mali zao. Hilo lilipokwisha, hawakuwa na kitu tena. Tofauti na hilo, maskini na waliokandamizwa waliweza kustahimili hali hiyo vizuri zaidi. Walikuwa wamezoea magumu na walikuwa wamekuza imani kubwa zaidi.

Wengi hufikiria kwamba mali inaweza kutosheleza mahitaji yao, huku wengine wakifikiri kwamba pesa zingetatua matatizo yao. Nimetembelea nchi maskini, na nimeona watu wakiishi kwenye vibanda vya nyasi na vitanda vilivyotengenezwa kwa majani ya migomba. Dhoruba inaweza kuharibu kijiji chao chote lakini watakusanyika ili kukijenga tena upya. Watu hawa huoga kwenye mito. Wanapika juu ya moto ambao upo wazi. Na wana furaha. Watoto wao wana furaha. Pia, nimeona mtu mcha Mungu kutoka kwenye mojawapo ya vijiji hivi akiharibiwa kabisa na pesa. Hakuwa muaminifu, mwenye ukaidi, na hata mwenye jeuri. Aliwatelekeza watoto wake. Sijawahi kuona mabadiliko makubwa zaidi kwa mtu. Pesa sio jibu. Badala yake, mara nyingi inaweza kusababisha matatizo mengi zaidi. Kutosheka kwa upande mwingine hutoa suluhu, na hupatikana kupitia mambo magumu na majaribu. Inapelekea mtu kumuamini Mungu kwa sababu hakuna mwingine wa kumuamini.

Wakati Paulo alipoletwa mbele ya Nero kwenye kesi yake, alisema: “bali

wote waliniacha". Lakini pia alisema: "Lakini Bwana alisimama pamoja nami, akanitia nguvu," 2 Timotheo 4:16-17. Shida na mateso huruhusu Mungu azijenge na kuzisafisha tabia zetu. Pale ambapo majaribu yanapokujia, kumbuka kuwa unaweza kuyashinda. Omba juu ya ahadi uliyopewa: "Nayaweza mambo yote katika Kristo anitiaye nguvu." Wafilipi 4:13. Kitabu cha Habakuki kina maelezo mengine yenye thamani kuhusu imani kwenye nyakati za majaribu.

> Habakuki 3:17 Maana mtini hautachanua maua, Wala mizabibuni hamtakuwa na matunda; Taabu ya mzeituni itakuwa bure, Na mashamba hayatatoa chakula; Zizini hamtakuwa na kundi, Wala vibandani hamtakuwa na kundi la ng'ombe;
> 3:18 Walakini nitamfurahia BWANA Nitamshangilia Mungu wa wokovu wangu.
> 3:19 YEHOVA, aliye BWANA, ni nguvu zangu, Yeye huifanya miguu yangu kuwa kama ya kulungu, Naye ataniendesha katika mahali pangu palipoinuka.

Wakati riziki yote ya Habakuki ilipotoweka mbele ya macho yake, alisema: "bado nitafurahi katika Bwana." Hii ni siri na baraka ya imani ya Kikristo. Kila mtu anapitia magumu, lakini Mkristo anapoyapitia, ana tumaini kwa Bwana. Ambapo kwa mtu aliyeasi, anachokiona tu ni hali mbaya iliyo mbele yake. Hana cha kutumainia na hakuna wa kumuamini. Wengi hukata tamaa na hata kujiua. Hata hivyo, Mkristo anaweza kupita jaribu iliyo mbele yake. Anajua kwamba anachovumilia ni cha muda tu na kuwa kuna maisha bora yajayo ambapo hakutakuwa na dhambi au mateso tena. Anajua kuwa siku inakuja ambayo "Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita." Ufunuo 21:4.

Tunapozingatia ahadi hizi, na kuweka macho yetu kwenye uzima wa milele, matatizo na majaribu yetu hufifia haraka sana. Bila shaka mstari unaofuata ndio andiko kuu zaidi katika Biblia yote kuhusu ni kwa nini Mungu anaruhusu mateso. Mtume Paulo aliteswa sana. Alipigwa mawe hadi pale wapinzani wake waliposadiki kwamba alikuwa amekufa. Alipigwa na kuvunjiwa meli mara nyingi, na bado anazungumza

juu ya mambo haya yote kama "mateso mepesi". Katika barua yake ya pili kwa kanisa la Wakorintho, tunasoma:

> 2 Wakorintho 4:17 Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; 4:18 tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele.

Paulo alidumisha mtazamo wa kuwa maisha yake duniani yalikuwa ni ya kitambo tu. Na alielewa kwamba dhiki "zinafanya kazi kwa ajili yetu" utukufu wa milele, kama vile matatizo ya Adamu yangekuwa "kwa ajili yako". Badala ya kuzingatia mambo yanayoonekana—majaribu na dhiki mbele yake—Paulo alichagua kuzingatia mambo ambayo hayaonekani—ahadi za Mungu na tumaini la uzima wa milele. Ukikumbuka vifungu hivi, na kuomba pale unapotaabika, majaribu yako pia yatakuwa ni mateso mepesi kwako. Hii inaweza hata kuwepo wakati mtu anapompoteza mpendwa wake, na ni kitu cha kiasili kukabiliwa na uchungu na huzuni. Kwa maana endapo anajua kwamba mtoto wako au mzazi alikuwa na haki mbele za Mungu, basi unajua pia kuwa utamuona tena. Na atajitahidi zaidi na zaidi kuhakikisha kwamba yupo sawa mbele za Mungu kwa sababu anataka kukaa mbinguni pamoja na mtu huyo milele. Kwa hivyo bila kujali dhiki ni nini, tunaweza kuwa na uhakika kwamba "inafanya kazi kwa ajili yetu". Kwa maana "Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake." Warumi 8:28.

Kwa hivyo, tukumbuke kuwa mateso hayatoki kwa Mungu. Na Mungu anafanya kazi kila wakati ili kutulinda na mateso, na kuhifadhi maisha yetu. Lakini wakati huo huo, mateso ni matokeo ya dhambi na uasi, na ni kwa manufaa yetu wenyewe kuwa tunakabiliana na matokeo ya matendo yetu mabaya. Tunapaswa kujifunza kutokana na matokeo haya na kujiepusha na dhambi. Kwa maana siku moja Mungu Ataweka ukomo wa mateso. Na Atakapofanya hivyo, itamlazimu kuweka ukomo wa dhambi na wa wenye dhambi pia. Kisha, hatimaye, hakutakuwa tena na maumivu, kuteseka, ukosefu wa haki, au kifo.

EARTHEN VESSELS

2 CORINTHIANS 4:7

www.earthenvessels.org.au
info@earthenvessels.org.au

NI KWA NINI MUNGU MWENYE UPENDO ANARUHUSU DHAMBI IWEPO?

NI KWA NINI KUNA MAUMIVU NA MATESO?

NI KWA NINI MUNGU HAINGILII KATI?

EARTHEN VESSELS
2 CORINTHIANS 4:7